

## **IKIWA UNADHANIA UMEKUMBANA NA TB**

Ikiwa unadhania umekuwa karibu na mtu aliye na ugonjwa wa TB, unapaswa kwenda kwa daktari wako au idara ya afya ili kupimwa TB.

## **Kwa habari zaidi kuhusu kifua kikuu kwenye wavuti, tafadhali tembelea:**

The Centers for Disease Control  
and Prevention  
[www.cdc.gov](http://www.cdc.gov)

U.S. Department of Health  
and Human Services  
[www.omhrc.gov](http://www.omhrc.gov)

• • •

*Habari ya brosha hii ilichukuliwa kutoka  
kwa nyenzo zilizotengenezwa na:*

*The Centers for Disease Control  
and Prevention (CDC)*

*U.S. Department of Health  
and Human Services*

*The Directors of Health Promotion  
and Education (DHPE)*

### **HABARI YA MAWASILIANO:**

[riht@uscridc.org](mailto:riht@uscridc.org)

**U.S. Committee for Refugees and  
Immigrants**

1717 Massachusetts Ave., NW  
Suite 200

Washington, DC 20036

Simu: 202 • 347 • 3507

Faksi: 202 • 347 • 7177

[www.refugees.org](http://www.refugees.org)

*Brosha hii ilitengenezwa na ufadhili kutoka kwa  
Idara ya Afya na Ofisi ya Huduma za Wanadamu  
ya Kuwapatia Wakimbizi makazi mapya.*



## **Je! Kifua kikuu ni nini? (What is Tuberculosis?)**

**(Swahili)**



[www.refugees.org](http://www.refugees.org)

*Protecting Refugees, Serving Immigrants,  
Upholding Freedom since 1911*

## JE! TB NI NINI?

Kifua kikuu, au “TB,” ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na vijidudu ambavyo vinaenezwa kupitia hewa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Mtu aliye na TB anaweza kufa kutokana ugonjwa huo ikikosa kutibiwa na madawa.

## TB INAENEZWA AJE?

Vijidudu vya TB huwekwa hewani wakati mtu aliye na TB anapokohoa, anapochafya, kuimba, kutema mate au kucheka. Watu wengine wanaopumua hewa iyo ambayo ina vijidudu vya TB wanaweza kuambukizwa.

## JE! NI NANI ANAYEPATA TB?

Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria kwamba karibu watu bilioni sita ulimwenguni kote wameambukizwa bakteria inayosababisha TB. Kila mwaka, karibu watu milioni mbili ulimwenguni kote hufa kutokana na TB. Watu ambao kila siku wanagusana na watu waliyo na TB wako kwa hatari ya kuambukizwa. Hii ni pamoja na wanafunzi wenza, wafanyikazi wenza, jamaa wa familia au wakaazi wenza.

## UGONJWA WA TB FICHE NI TOFAUTI AJE NA TB HAI?

Watu waliyo na TB fiche wana bakteria ambayo inasababisha TB katika miili yao lakini

bakteria hiyo si hai na watu hao si wagonjwa. Watu waliyo na TB fiche hawawezi kupitisha TB kwa wengine, lakini wanaweza kuwa na TB hai katika maisha ya baadaye.

Watu waliyo na TB hai wana ugonjwa wa TB. Hii inamaanisha kwamba bakteria ambayo inasababisha TB inazaana sana na kuharibu tishu mwilini. Watu waliyo na ugonjwa wa TB wana dalili za TB na wanaweza kupitisha ugonjwa huo kwa wengine, haswa watu wanao waona kila siku kama vile wafanyikazi wenza, wanafunzi wenza, na jamaa wa familia.

## TB INAYOKINZA MADAWA

Mtu aliye na TB akikosa kuchukua madawa yake vizuri, au akiwacha kutumia madawa haraka sana, vijidudu vinavyosababisha TB vinaweza kinza madawa hayo. Hiyo inamaanisha madawa hayo hatafanya kazi tena, ambayo inamaana kwamba itambidi mtu huyo kupewa madawa tofautu - yaliyo na nguvu zaidi- kwa muda mrefu zaidi ya vile ingechukua kumaliza matibabu asili. TB inayokiza madawa ni ngumu na inagharimu zaidi kutibu.

## TB INATIBIWA AJE?

TB INAWEZA KUPONYWA! Inachukua muda mrefu zaidi kutibu TB. Wagonjwa wa TB lazima watumie madawa kadhaa kwa miezi 6 hadi 12 ili kutibu ugonjwa huo. Mtu aliye na TB anaweza kuhisi nafuu kabla ya utabibu kumalizika. Uaminifu—kutumia madawa yote ya TB kama ilivyoagizwa hadi yaishe—ni muhimu kwa kuponya TB. Mtu aliye na TB akiacha kutumia madawa kabla ya utabibu kuisha, anaweza kuwa mgonjwa tena.

